

JAMHURI YA MUUNGANO TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM



Kumb. Na.DCC/CP.4/4

19/09/2022

TANGAZO LINARUDIWA

TANGAZO LA NAFASI YA MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA YA HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM KWA KIPINDI CHA MWAKA 2022 HADI 2025

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam anawatangazia Wananchi kuwa kuna nafasi wazi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira ya Halmashauri ya Jiji kwa kipindi cha miaka mitatu 2022 hadi 2025.

SIFA ZA MWOMBAJI

1. Awe ni raia wa Tanzania na mkazi wa Dar es Salaam
2. Awe na angalau Shahada ya Kwanza katika fani Utawala, Sheria na Sayansi ya Jamii
3. Awe na akili timamu
4. Asiwe amewahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai
5. Asiwe na Wadhifa wa Kisiasa au uongozi wa ngazi yoyote katika Chama cha Siasa
6. Asiwe mtumishi wa Umma


TARATIBU ZA KUWASILISHA MAOMBI

1. Waombaji wote watume barua za maombi zikiwa na viambatisho vifuatavyo:
 - i) Nakala iliyothibitishwa ya cheti cha kuzaliwa au kitambulisho cha Taifa (Certified copy)
 - ii) Nakala zilizothibitishwa za vyeti vya masomo na Taaluma (Certified copies)
 - iii) Barua ya utambulisho toka kwa Mwenyekiti wa Serikali za Mitaa anapoishi ikiwa na picha ndogo ya hivi karibuni
 - iv) Wasifu binafsi (CV)
 - v) Barua toka kwa Wadhamini wawili (2) zikiwa na anuani kamili Email.

NB: Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 26 Septemba, 2022

Barua zote za maombi zitumwe kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi wa Jiji
1 Mtaa wa Mission
S.L.P. 20950
Halmashauri ya Jiji
11883 – DAR ES SALAAM



Eng. Amani I. B. Mafuru

KAIMU MKURUGENZI WA JIJI